**MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA TAREHE 03/05/2017 HADI 04/05/2017**

**Mahudhurio**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. | Kashunju S.R | Mwenyekiti |
| 2. | Mh. | Jonas T. Vedasto | Mjumbe |
| 3. | Mh. | Said Abdunuru | Mjumbe |
| 4. | Mh. | Theophila K. Theobard | Mjumbe |
| 5. | Mh. | Henery F. Bashasha | Mjumbe |
| 6. | Mh. | Gaspary B. Gabriel | Mjumbe |
| 7. | Mh. | Hasanat M. Chamani | Mjumbe |
| 8. | Mh. | Sadath Jeremiah | Mjumbe |
| 9. | Mh. | Devotha Nestory | Mjumbe |
| 10. | Mh. | Hyasintha T. Katita | Mjumbe |
| 11. | Mh. | Restuta K. Kafuba | Mjumbe |
| 12. | Mh. | Sevelini P. Bugoha | Mjumbe |
| 13. | Mh. | Byarufu R. Beneth | Mjumbe |
| 14. | Mh. | Benan L. Rwabalema | Mjumbe |
| 15. | Mh. | Ernest Kalisa | Mjumbe |
| 16. | Mh. | Angelo G. Rwaibebe | Mjumbe |
| 17. | Mh. | Fulgence M. Frederick | Mjumbe |
| 18. | Mh. | Bahati Heneriko | Mjumbe |
| 19. | Mh. | Consolatha Kanyima | Mjumbe |
| 20. | Mh. | Daud S. Mashurano | Mjumbe |
| 21. | Mh. | Prudence Mweyunge | Mjumbe |
| 22. | Mh. | Joel S. Nshobeilwe | Mjumbe |
| 23. | Mh. | Emmanuel N. Alfred | Mjumbe |
| 24. | Mh. | Jovinary K. John | Mjumbe |
| 25. | Mh. | Devotha M. Byashara | Mjumbe |
| 26. | Mh. | Joyleth G. Mutashaga | Mjumbe |
| 27. | Mh. | Clepin R. Bernard | Mjumbe |
| 28. | Mh. | Eustace L. Christian | Mjumbe |
| 29. | Mh. | Tulakira L. Twijuke | Mjumbe |
| 30. | Mh. | Laurean M. Simon | Mjumbe |
| 31. | Mh. | Kimalala G. Eustace | Mjumbe |
| 32. | Mh. | Majaliwa John | Mjumbe |
| 33. | Ndg. | Shadrack M. Mhagama | Katibu |

**Wasiohudhuria**

| | |
|---|---|
| Mh, Innocent Bilakwate (mb) | Kwa taarifa |

**Waalikwa**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Col (rtd) Shaban I. Lissu | Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa |
| 2. | Clemence R. Kafuba | Mwenyekiti CCM (W) |
| 3. | Odilia Maholelo | Katibu CCM (W) |
| 4. | Bazil Waziri | Katibu CHADEMA (W) |
| 5. | Rachel Mkama | Mwandishi wa Habari FADECO Redio |
| 6. | Ezra Lugakila | Mwandishi wa Habari Karagwe FM |
| 7. | Nuhu Badiru | Sheikh wa Wilaya |
| 8. | ASP G.C Kyekaka | Afisa Magereza |
| 9. | SR. Liberatha Mkanoel | Kny: Paroko Isingiro |
| 10. | Paul M. Stephen | Afisa uhamiaji waWilaya |
| 11. | Greyson I. Mwengu | Katibu Tawala waWilaya |
| 12. | Robert J. Marwa (ASP) | Mkuu wa Polisi Wilaya Kyerwa |
| 13. | Elias Joseph | Afisa Usalama wa Taifa waWilaya |
| 14. | CAPT A. D Ndelwa | DMA |
| 15. | Rev. Yaredi Wakami | Mchungaji E.L.C.T |
| 16. | Anna H. Kapwela | Afisa usajili (NIDA) |

**Wataalam:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Stephen Sindagulu | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 2. | Francis L. Nshaija | Mkuu wa Idara ya elimu sekondari |
| 3. | Scarion Kagaruki | Kaimu afisa mtendaji wa kata Kitwechenkura |
| 4. | Ladislaus K. Odilo | Kny: Mtendaji wa kata-Isingiro |
| 5. | Audax E. Byekwaso | Mtendaji wa kata- Rwabwere |
| 6. | Evodia F. Kapere | Mtendaji wa kata- Songambele |
| 7. | Josiah Mambo | Mtendaji wa kata- Murongo |
| 8. | Yassin Juma | Afisa uvuvi |
| 9. | Deus C. Korongo | Mtendaji wa kata- Nyakatuntu |
| 10. | Swalehe Ntakisigaye | Mtendaji wa kata- Kimuli |
| 11. | Pontian Nestory | Kaimu afisa Mtendaji wa kata- Kitwe |
| 12. | Faustine Mboineki | Afisa mazao |
| 13. | Musa A. Jumanne | Afisa tarafa Mabira |
| 14. | Emmanuel Lyanga | Mratibu TASAF III |
| 15. | Juma Magotto | Mkuu wa Idara ya Ujenzi na Zimamoto |
| 16. | Aaron Vedasto | Kaimu mkuu wa Idara ya elimu msingi |
| 17. | Meshack A. Libent | Mkuu wa idara ya kilimo, ushirika na umwagiliaji |
| 18. | Evarista Chacky | Afisa usafirishaji |
| 19. | Prosper Rutakinikwa | Kaimu mkuu wa idara ya maendeleo ya mifugo na uvuvi |
| 20. | Simon D. Charles | Kny: Mkuu wa idara ya maji |
| 21. | Paschal Rwamugata | Mtendaji wa kata- Kibale |
| 22. | Osward Makanzu | Mtendaji wa kata- Kyerwa |

| | | |
|---|---|---|
| 23. | Remmygeus B. Basimaki | Mtendaji wa kata- Bugomora |
| 24. | Novatus Kajoki | Kaimu afisa mtendaji wa kata Nyaruzumbura |
| 25. | Christopha K. Theonest | Mtendaji wa kata –Kamuli |
| 26. | Longino F. Balyalemwa | Kny: Mtendaji wa kata-Mabira |
| 27. | Yoweli T. Barthurumeo | Kaimu afisa Mtendaji wa kata Bugara |
| 28. | Joachim Justinian | Mtendaji wa kata Rutunguru |
| 29. | Theophil Kweyamba | Mratibu wa Mwenge |
| 30. | Nicholaus P. Rugemalira | Afisa tarafa Murongo |
| 31. | Obed A. Kamwela | Mkaguzi wa kahawa |
| 32. | Pontian Bahesha | Kaimu afisa Mtendaji wa kata- Kikukuru |
| 33. | Francis M. Frednand | Kaimu afisa Mtendaji wa kata-Nkwenda |
| 34. | Mussa Omari | Kny: Mtendaji wa kata – Kaisho |
| 35. | Dickson P. Mutensa | Kny: Mtendaji wa kata- Kakanja |
| 36. | Francis Mwita | Afisa Utumishi |
| 37. | Dr. Diocles Ngaiza | Kaimu Mganga mkuu wa Wilaya |
| 38. | Bernard Ngatunga | Kny: Mkuu wa kitengo cha ukaguzi wa ndani |
| 39. | Richard Mayiku | Kaimu Mkuu wa idara ya ardhi na maliasili |
| 40. | Joanitha N. Balthazari | Afisa Utumishi |
| 41. | Bugingo Frolent | Kny: Mkuu wa Idara ya mipango, takwimu na ufuatiliaji |
| 42. | M.Z Mtafungwa | Afisa tarafa Nkwenda |
| 43. | Peter Rutaba | Afisa mifugo |
| 44. | Golden Nzalalila | Mratibu Maafa |
| 45. | Francis Mwita | Afisa Tawala |
| 46. | Simeon Bairu | Mtendaji wa kata Iteera |
| 47. | Josephat Ishengoma | Dereva |
| 48. | Vicent Prospery | Kny:Mtendaji kata ya Kibingo |
| 49. | Mang’oha J. Maginga | Mkuu wa Idara ya utawala na utumishi |
| 50. | Lazaro Majeta | Kaimu mkuu wa idara ya maendeleo ya jamii ustawi wa jamii na maendeleo ya vijana |
| 51. | Asheri Mtango | Katibu wa Afya |
| 52. | Alex Kagande | Mkuu wa kitengo cha manunuzi ya umma na ugavi |
| 53. | Norah P. Nyakunga | Afisa lishe |
| 54. | Lumumba A | Afisa kilimo |
| 55. | Fulgence B. Bishashara | Kny: Afisa tarafa Kaisho |
| 56. | Yasin S. Mwinory | Kaimu mkuu wa idara ya usafi na mazingira |
| 57. | Deus Bagenyi | Dereva |
| 58. | Zephrine Kabona | Katibu TSC |
| 59. | Jovin Rutainulwa | Afisa sheria |
| 60. | Rocky Kafuba | Kny: Mtendaji Kata Rukulaijo |

**Sekretarieti:**
Ildephonce Valentine
Asimwe Henery
**Agenda:**

**SIKU YA KWANZA JUMATANO, TAREHE 03/05/2017**

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha dondoo
3. Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli kutoka kwa Wenyeviti wa Maendeleo ya kata (WDC)

**SIKU YA PILI ALHAMISI, TAREHE 04/05/2017**

4. Taarifa ya Mwenyekiti wa Halmashauri akifungua rasmi mkutano wa Baraza la madiwani Mei, 3 – 4/5/2017.
5. Maelekezo ya Serikali
6. Maswali ya papo kwa papo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya
7. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 29-30/01/2017
8. Utekelezaji wa maazimio kikao kilichopita cha tarehe 29-30/01/2017
9. Kupokea taarifa ya Utendaji wa Uwajibikaji wa Halmashauri kutoka kwa Wenyeviti wa Kamati za kudumu kwa kipindi cha robo ya tatu 2016/2017
   i) Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango
   ii) Kamati ya Elimu, Afya na Maji
   iii) Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
   iv) Kamati ya kudhibiti UKIMWI
10. Taarifa za Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya
   i) Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2016/2017
   ii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ndani kwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2016/2017
   iii) Taarifa ya Manunuzi na Bodi ya Zabuni kwa robo ya tatu kuanzia Januari hadi Machi, 2016/2017
   iv) Taarifa ya Kitengo cha Sheria robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2016/2017

11. Taarifa zinginezo muhimu
   i. Taarifa ya hali ya Usalama ya Wilaya
   ii. Taarifa ya hali ya uhamiaji
12. Kufunga kikao.

**KUMB NA 23/2016/2017 KUFUNGUA KIKAO**

Katibu wa kikao alieleza kuwa kikao hiki ni kikao cha kazi, alifanya utambulisho kwa wajumbe na wageni waliohudhuria. Alimkaribisha mwenyekiti kufungua kikao, Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kueleza kuwa katika vikao vya kawaida vya baraza la madiwani pamoja na kamati za kudumu hakuna mjumbe yeyote anayeruhusiwa kuvaa sare ya chama. Baada ya kusema hayo alifungua kikao mnamo saa 5:05 asubuhi.

**KUMB NA 24/2016/2017 KUTHIBITISHA DONDOO**

Dondoo zilithibitishwa kama zilivyowasilishwa na kuongeza agenda ya "taarifa ya hali ya uhamiaji" na kuwa dondoo namba 11 (ii).

**KUMB NA 25/2016/2017 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO YA KATA (WDC) KUTOKA KWA WENYEVITI WA KATA**

Taarifa za kata ziliwasilishwa kama ifuatavyo:-

1. Kata Rukulaijo: Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.
2. Kata Kamuli: Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.
3. Kata Rutunguru: Taarifa iliwasilishwa na kueleza kuwa bado kuna changamoto ya madawati katika shule ya sekondari Nyabishenge.
4. Kata Kitwechenkura: Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kama ifuatavyo:-

**Hoja:** Michango inayotolewa katika shule ilipatiwa kibali?

**Ufafanuzi:** Ilijibiwa kuwa kwenye suala la kibali maelekezo hayajatolewa.

**Hoja**: Mjumbe alihitaji kupata ufafanuzi jinsi mipaka ya ardhi ya vijiji ilivyogawiwa.

**Ufafanuzi**: Ulitolewa ufafanuzi kwamba mipaka iligawiwa kwa kufuata taratibu za vikao vya Serikali ya kijiji vyenye mamlaka ya kugawa ardhi. Pia ziliwekwa alama asilia za minyaa kwenye mipaka iliyobainishwa.

5. Kata Kaisho:

Taarifa iliwasilishwa na kutolewa ombi la kupewa Mtendaji wa kata kwani kata hiyo haina mtendaji wa Kata.

**Hoja**: Kuna mpango gani wa kujenga vibanda vya kliniki katika kata ya Kaisho?

**Ufafanuzi**: Vibanda vilishaanza kujengwa, vimejengwa vibanda viwili na kibanda kimoja kilichobaki kitakamilika muda wowote.

Ulitolewa ushauri kuwa ni vizuri fedha ya “captation grants” kutolewa taarifa jinsi inavyotumika kwa sababu kuna baadhi ya shule hawatoi taarifa ya fedha hizo.

**Azimio, wataalam ngazi ya kata wahudhurie vikao vya kamati ya maendeleo ya kata (WDC) na kutoa utaalam unaotakiwa katika sekta zao.**

6. **Kata Iteera:** Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa
7. **Kata Mabira:** Taarifa iliwasilishwa na kushauriwa kufunguliwa akaunti ya shule ya sekondari Mabira ambayo haifanyi kazi.
8. **Kata Nyakatuntu:** Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kama ifuatavyo:-

**Hoja:** Ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya msingi Kyereta umefikia hatua gani?

**Ufafanuzi:** Ilijibiwa kuwa jengo limefikia hatua ya uezekaji**.**

9. **Kata Isingiro:**

**Hoja: N**i lini chumba cha darasa katika shule ya sekondari Isingiro kitakamilika?

**Ufafanuzi: C**humba cha darasa kitakamilika baada ya siku 8 tangu tarehe ya kikao hiki.

10. **Kata Murongo:** Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kama ifuatavyo:-

**Hoja:** Kuna mpango gani wa kuanzisha vyumba vya madarasa shule ya msingi Kashenyi kwa uhitaji uliopo?

**Ufafanuzi:** Vikao vimeishafanyika na mchango ulikwishapitishwa hivyo wananchi wakichangia ujenzi utaanza mara moja**.**

**Hoja:** Kuna mpango gani wa kudhibiti magendo ya kahawa mpakani?

**Ufafanuzi:** Utaratibu wa kudhibiti umeishaanza isipokuwa ni kuongeza nguvu ya wanamgambo ili kuimarisha udhibiti ulio imara.

11. **Kata Kimuli:** Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kama ifuatavyo:

**Hoja:** Mihtasari ya vikao vya vitongoji inawasilishwa katani**?**

**Ufafanuzi**: Mihtasari haiwasilishwi kama ilivyopangwa.

Ilishauriwa ufanyike uteuzi wa mtumishi mmoja atakayeshughulikia mihtasari ya vijiji na vitongoji.

Ilielezwa kuwa fedha zinazotolewa kwenye kata baadhi ya Watendaji wa kata awakiri kupokea stakabadhi za mapokezi ya fedha zinazotolewa. Iliagizwa kuwa zitolewe stakabadhi za kukiri mapokezi ya fedha zinazotolewa Katani ndani ya wiki mbili tangia tarehe ya kikao hiki.

**Azimio: Zitolewe stakabadhi za kukiri mapokezi ya fedha zinazotolewa katani ndani ya wiki mbili tangia tarehe ya kikao hiki.**

12. **Kata Kyerwa**: Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.
13. **Kata Songambele**: Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kama ifuatavyo:-

**Hoja**: Kuwa madeni yaliyokopwa shule ya sekondari Chanyangabwa kuna hatua gani zilikwishachukuliwa?

**Ufafanuzi:** Ilijibiwa kuwa Mheshimiwa Diwani aliyetangulia hakuacha taarifa ya mapato na matumizi hivyo deni halikubainishwa.

14. **Kata Bugomora**: Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.
15. **Kata Nyaruzumbura**: Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kama ifuatavyo:-

**Hoja**: Mjumbe alipenda kupata taarifa kutoka kwa afisa elimu sekondari kama ameisha tembelea shule ya sekondari Nyaruzumbura.

**Ufafanuzi**: Ilijibiwa kuwa bado shule haijatembelewa kwa kuwa taarifa zimefika shule itatembelewa.

16. **Kata Nkwenda**: Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.
17. **Kata Kikukuru:** Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.
18. **Kata Kitwe:** Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.
19. **Kata Kibare:** Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kama ifuatavyo:-

**Hoja**: Ni kwa nini mikutano ya kudhibiti UKIMWI ngazi ya vijiji haifanyiki?

**Ufafanuzi**: Ni kweli mikutano haikufanyika kwa robo hii, kwa robo inayofuata mikutano hiyo itafanyika.

**Hoja**: Kwa nini fedha ya "P4R" iliyotolewa kujenga chumba cha darasa katika shule ya msingi Rulama haijatolewa taarifa?

**Ufafanuzi**: Ilijibiwa kwamba fedha hiyo ilipokelewa mwezi Aprili, 2017 na taarifa ilikuwa tayari imeandaliwa hivyo itatolewa kikao kinachofuata.

**Azimio**, **Itolewe taarifa ya mapato na matumizi kwa kata zote zilizopokea fedha ya "P4R".**

20. **Kata Kakanja:** Tarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kama ifuatavyo:-
    **Hoja:** Kuna utaratibu gani wa kukamilisha madawati ambayo hayajakamilika?
    **Ufafanuzi:** Madawati yaliyobaki yatatengenezwa kwa kushirikiana kwa kata mbili Kata Kakanja na kata Kimuli, katika vikao walivyokaa walikubaliana kila mzazi mwenye mwanafunzi kuchangia madawati na siyo jamii nzima.

**Azimio**, **zilitolewa siku 14 ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kupata mrejesho wa ukamilishaji wa madawati ya shule ya Sekondari Kimuli kutoka kata ya Kakanja.**

21. **Kata Rwabwere**: Taarifa iliwasilishwa na kutolewa ombi la ofisi ya ardhi kutembelea mipaka ya Rwabwere na Nkwenda ili kupata eneo la kujenga shule. Lilitolewa agizo la kutembelea eneo hilo ili ujenzi uweze kuendelea.

    **Azimio**, **Zilitolewa siku 14 kutembelea mipaka ya kata ya Rwabwere na Nkwenda na kumaliza tatizo ili shughuli za maendeleo ziweze kuendelea**.
22. **Kata Bugara**: Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kuwa,

    **Hoja**: Ni utaratibu gani unatumika kuchangia madawati katika shule ya sekondari Businde?.

    **Ufafanuzi**: Ilijibiwa kuwa kupitia vikao halali walikubaliana wazazi wenye wanafunzi katika shule hiyo watachangia madawati kwani kata ya Bugara wapo kwenye mpango wa kujenga shule ya kwao.
23. **Kata Businde**: Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.
24. **Kata Kibingo**: Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.

Baada ya kata zote kuwasilisha taarifa ilielezwa kuwa watendaji wa kata walioandikiwa barua ya kutenga maeneo kwenye vijiji kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo linafanyiwa kazi kikamilifu.

Kikao kiliahirishwa mnamo saa 10:08 jioni.

**SIKU YA PILI TAREHE 4/5/2017**

**KUMB NA 26/2016/2017 TAARIFA YA MWENYEKITI WA HALMASHAURI AKIFUNGUA RASMI MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI MEI, 3 – 4/5/2017**

Katibu alieleza kuwa ni kikao cha robo ya tatu kwa mwwaka wa fedha 2016/2017. Alimkaribisha mwenyekiti kufungua kikao, mwenyekiti alianza kwa kutoa pole kwa msiba uliotokea wa watu wawili waliokufa maji katika mto Kagera. Baada ya kusema hilo alitoa hotuba yake ya ufunguzi kama ifuatavyo:-

Hali ya chakula Wilaya ya Kyerwa kwa sasa hivi inaridhisha. Pia alieleza kuwa mbegu na mbolea zitolewe kwa wakulima kabla ya kupanda ili mazao yatakayopandwa kuwa na ubora.

Katika hotuba yake alieleza kuwa Wilaya ya Kyerwa ina nyanda za malisho kama vile Ruhita, Katabe, Siina na Buyanja lakini mbunga hizo za hifadhi zimevamiwa na wakulima. Hivyo nyanda hizo zipimwe na watakaotaka kutumia wapewe “block” ambazo watazilipia na kuzitunza kwa matumizi yatakayokuwa yanaendelea.

Ulitolewa ushauri kuwa wananchi waliovamia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya hifadhi waondolewe.

Matengenezo ya barabara, alieleza kuwa zimetolewa Tshs. 1,889,470,000.07 kwa matengenezo ya barabara ya Isingiro - Ishaka na barabara ya Nyabishenge - Rwengoha. Alimpongeza

Mkurugenzi Mtendaji na timu yake ya menejimenti kusimamia miradi ya barabara. Pia katika hotuba yake alitoa taarifa kuwa ujenzi wa jengo la Halmashauri mkandarasi ameishapatikana na ujenzi utaanza ndani ya mwezi Mei, 2017.

Aliendelea kueleza kuwa ujenzi wa nyumba mbili (2) za watumishi eneo la Rwenkorongo unaoendelea vizuri.

Alieleza kuwa huduma za afya zinaendelea kutolewa vizuri ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa. Alisisitiza kuhimiza wananchi kujiunga mfuko wa bima ya Afya kwa wale ambao hawajajiunga.

Katika sekta ya maji, aliomba waheshimiwa madiwani kutoa ushirikiano kwa mkandarasi na kutunza vyanzo vya maji kwa kuelimisha wananchi kutofanya kilimo au shughuli nyingine yoyote ndani ya mita 60.

Sekta ya elimu, fedha iliyotolewa kwa kutekeleza miradi mbalimbali itumike kama ilivyoelekezwa. Ulitolewa ushauri kwa afisa maendeleo ya jamii kukusanya takwimu za watu wenye mahitaji maalum ili waweze kuingizwa kwenye bajeti.

Ilielezwa kuwa Wilaya ya Kyerwa bado ipo nyuma katika kupanda miti rafiki kwenye milima. Aidha lilitolewa ombi la kuongeza nguvu kazi kwa kutumia askari mgambo kuhakikisha milima inapandwa miti.

**Azimio**, **Kila kijiji kiwe na kitalu cha miti na kupanda miti ambayo ni rafiki.**

Baada ya kutoa hotuba alifungua kikao rasmi mnamo saa 5:40 asubuhi.

**KUMB NA 27/2016/2017 MAELEKEZO YA SERIKALI**

Yalitolewa maelekezo ya Serikali kama ifuatavyo:-

Katika ombi la kutumia askari mgambo kusaidia kupanda miti, ilielezwa kuwa wabainishwe askari mgambo kila kata ili kuweza kuwatumia katika zoezi hilo.

Katika jambo la ulinzi na usalama ilielezwa kwamba viongozi wote ngazi ya chini yaani Kata, Vijiji na Vitongoji wanapaswa kuwa na ushirikiano ili kuhakikisha amani ipo na kuwaletea wananchi maendeleo.

Pia yalitolewa maelekezo kuwa wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao hawajaripoti shuleni ufanyike ufuatiliaji na kuhakikisha wanafunzi wote wanaripoti shuleni.

Aliagizwa Mkurugenzi Mtendaji kufuatilia maafisa ugani ngazi ya kata ili waweze kuwajibika katika nafasi zao. Vilevile alisisitiza kuwa kila mwananchi anapaswa kuwa na choo bora.

Liliongelewa suala la viongozi kuwa wazalendo katika kulinda kahawa isivushwe kupelekwa nchi jirani ya Uganda.

Baada ya taarifa ya Mwenyekiti na maelekezo ya Serikali wajumbe walihoji kama ifuatavyo:-

**Hoja**: Kuna utaratibu gani kwa wananchi wanaoshindwa kuchangia michango ya maendeleo?

**Ufafanuzi:** michango itakayowekwa isiwe ya kudumu, utaratibu wa Serikali ni kufuata taratibu zinazotakiwa yaani kupitia kwenye vikao na mikutano na kukubaliana michango itakayochangwa. Pia michango shuleni ni kuandaa mihtasari ya mikutano na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji ili awasilishe maombi ya kupewa kibali kutoka kwa Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) kuruhusu michango waliokubaliana.

Lilitolewa ombi la kijiji cha Rwamashaju kuingizwa kwenye mpango ili kupatiwa maji. Yalitolewa maelezo kwamba litafuatiliwa kama kijiji kipo kwenye mpango litatekelezwa na kama hakipo kwenye mpango kitaingizwa kwa mwaka wa fedha unaofuata.

**KUMB NA 28/2016/2017 MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

Yaliulizwa maswali ya papo kwa papo kama ifuatavyo:-

1. Joel Nshobeilwe
   **Swali**: Ni lini itajengwa kalvati mpakani mwa Kata ya Nyakatuntu na Nyaruzumbura?
   **Jibu**: Litaingizwa katika bajeti kwa mwaka wa fedha unaofuata.
2. Sevelin P. Bugoha
   **Swali**: Ni lini umeme utaletwa Kata ya Murongo?
   **Jibu**: Mkuu wa Wilaya atafuatilia na kujua hatima yake.
3. Bahati Henerico:
   **Swali**: Kwa nini Mkurugenzi Mtendaji hajatembelea majengo yaliyokabidhiwa na World Vision?
   **Jibu:** Majengo yalitembelewa na kukubaliana yaanze kutumika kwa wanafunzi wa awali na chekechea. Pia chumba kimojawapo kitakuwa ni ofisi ya Mtendaji wa kata ya Rwabwere.
   Mjumbe alihitaji kupata ufafanuzi wa majengo yanayotumiwa na shule ya msingi KIDO kuwa ni ya nani. Ulitolewa ufafanuzi kuwa awali majengo hayo yalitumiwa na Baraza la Bakwata, suala hili lifanyiwe ufuatiliaji na kubaini ni nani anayeyatumia kwa sasa.
4. Hyasinta Katita
   **Swal**i: Ni lini agizo la kupelekwa 20% katika vijiji litatekelezwa?
   **Jibu**: Hakuna utaratibu maalum wa kupeleka 20% kwenye vijiji isipokuwa inatolewa kulingana na makusanyo kutoka kila kijiji. Katika kutekeleza hilo vijiji vyote vilivyowasilisha makusanyo viliwekewa fedha kufikia tarehe 15/04/2017.
5. Devotha Byashara
   **Swali**: Ni lini Halmashauri itatoa elimu kwa akina mama na vijana katika uzalishaji mali?
   **Jibu**: Vikundi ambavyo vina miradi na vitakavyoundwa kwa lengo la uzalishaji mali vitapatiwa elimu juu ya ujasiliamali. Kwa sasa hivi Halmashauri imeanza na kikundi cha vijana sekido Mabira.

6. Hasanath Chamani

   **Swali:** Ni lini barabara ya kutoka Mabira hadi Kyerwa itatengenezwa?

   **Jibu**: Barabara ya Mabira hadi Kyerwa kwa sasa hivi imerudishwa "tanroad" kwa kuwa barabara hiyo iliwekwa kwenye mpango wa mwaka 2016/2017 kama patahitajika matengenezo kabla ya "tanroad" kufanya matengenezo Halmashauri itafanya marekebisho yatakayojitokeza.

7. Frederick Fulgence

   **Swali**: Maeneo yaliyochukuliwa na eneo la Magereza ni lini wananchi wa maeneo hayo watapewa fidia?

   **Jibu**: Eneo lililotwaliwa na eneo la magereza ilielezwa kuwa, taratibu za malipo zinaendelea kwa kamishna wa magereza. Hivyo ilishauriwa kuwa wananchi wawe na subira taratibu zikikamilika watalipwa fidia zao.

8. Clepin Bernard

   **Swali**: Vitongoji vilivyoorodheshwa kupatiwa umeme wa REA kwa awamu ya III ni lini vitapatiwa umeme?

   **Jibu**: Ilielezwa kuwa zoezi lilipaswa kuanza Februari, 2017 lakini baadhi ya wasambazaji wa umeme waliingia kijanja jambo ambalo lilipelekea kuteuliwa wengine na zoezi linaweza kuanza Juni, 2017.

9. Ernest Kalisa

   **Swali**: Ni lini itajengwa stendi ya magari katika mji wa kibiashara wa Isingiro?

   **Jibu**: Shughuli ilishaanza kwani iliteuliwa timu ya kubaini maeneo yatakayokuwa yanafaa katika eneo la Isingiro. Pia mpango uliopo ni kupata stendi katika makao makuu ya Wilaya Rubwera pamoja na mji mdogo wa Nkwenda.

10. Gaspary B. Gabriel

    **Swali**: Ni lini kalvati ya mpakani wa Bugara na Mabira itatengenezwa? Kwani kipindi cha mvua hakuna mawasiliano katika kata hizo mbili.

    **Jibu**: Taarifa ilikuwa haijatolewa hivyo limepokelewa na litafanyiwa kazi.

11. Beneth Byarufu

    **Swali**: Kwa nini uhamisho wa walimu hauzingatii idadi ya wanafunzi?

    **Jibu**: Ugawaji wa walimu unazingatia uwiano wa mwalimu na wanafunzi ambapo vijijini ni mwalimu 1kati ya wanafunzi 50.

**KUMB NA 29/2016/2017 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 29 HADI 30/01/2017**

Muhtasari ulisomwa na kufanyiwa masahihisho kama ifuatavyo:-

Ukurasa wa 17 neno afisa kuanza kwa herufi kubwa na ukurasa wa 18 neno mauji liandikwe mauaji. Baada ya masahihisho hayo muhtasari ulisainiwa na kuwa kumbukumbu halali.

**KUMB NA30/2016/2017 UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 29 HADI 30/01/2017**

**Hoja**: Sheria zote za kutunza mazingira zifuatiliwe na kuanza kufanya kazi

**Utekelezaji**: Utekelezaji wa sheria ya mazingira umefanyika katika maeneo manne (4) kama ifuatavyo:
(i) **Ujenzi wa vyoo bora:** zimeanishwa jumla ya kaya 4298 kati ya 61339 hazina vyoo bora na maelekezo yametolewa kuwa ifikapo juni 30 wawe wamekamilisha ujenzi wa vyoo bora.
(ii) **Maeneo ya vyanzo vya maji**:
(a)Eneo lenye jumla ya ekari 73 katika vyanzo vya maji vilivyopo kata ya Kitwe lilikuwa limevamiwa na wananchi kwa kupanda mazao ya ndizi na kahawa. Wananchi wameondolewa katika eneo hilo na eneo limepandwa miti rafiki kwa njia shirikishi.
(b) Kuhifadhi mazingira kwa kurudisha uoto wa asili katika vyanzo vya maji vinne (4) ambavyo ni : Mtugunda, Kanoni, Masheshe na Msisha.
(iii) **Uhamasishaji wa upandaji miti**. Kila kata imehamasishwa kupanda miti.Jumla ya miti 9200 imepandwa kama shamba darasa katika kata za Kakanja na Isingiro Kijiji cha Karukwanzi.
(iv) **Kuainisha maeneo ya milima na kuyahifadhi kwa kuyapanda miti**. Iliandikwa barua yenye kumb Na.BE.352/499/20/31 ya tarehe 9/11/2016 kwa watendaji wote wa kata kuainisha maeneo ya milima ili ihifadhiwe kwa kupandwa miti.

**Hoja**: Ratiba za vikao zifuatwe kama zilivyopangwa

**Utekelezaji**: Ratiba imefanyiwa marekebisho kwa kuzingatia ratiba ya mikutano ya Bunge. Ratiba imeambatishwa na kablasha la mkutano wa Baraza la madiwani

**Hoja**: Kata ya Kakanja, Kibare, Kikukuru na Kitwechenkura wachukuliwe hatua za kisheria kwa kushindwa kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya kata kwa robo ya pili 2016/2017
**Utekelezaji**: Watendaji wa kata wameandikiwa barua za kujieleza kama ifuatavyo:
-Mtendaji wa Kata ya Kitwechenkura ameandikiwa barua yenye Kumb. Na. KGR/HW/KYR/JB.205/13 ya tarehe 21/04/2017
-Mtendaji wa Kata ya Kikukuru ameandikiwa barua yenye Kumb. Na. KGR/HW/KYR/JB.61/20 ya tarehe 21/04/2017
- Mtendaji wa Kata ya Kakanja ameandikiwa barua yenye Kumb. Na. KGR/HW/KYR/JB.863/25 ya tarehe 21/04/2017
- Mtendaji wa Kata ya Kibare ameandikiwa barua yenye Kumb. Na.KGR/HW/KYR/JB.38/28 ya tarehe 21/04/2017. Na taratibu za kinidhamu zinaendelea.

**HOJA**: Ateuliwe Afisa Ardhi na kuwezeshwa kufuata hati miliki za viwanja vya wananchi.
**UTEKELEZAJI**: Kamishina wa ardhi ametoa utaratibu kuwa wananchi watakuwa wanachukua hatimiliki zilizosajiliwa Mkoani. Mamlaka za Halmashauri zitakuwa zinajulishwa idadi ya hati zilizosajiliwa ili wajulishwe wananchi kufuata hatimiliki baada ya kuletwa na kamishina mkoani. Hata hivyo haimzuii mwananchi kufuata hati yake kwa msajili Mwanza pale ambapo hati zitakuwa hazijaletwa mkoani. Kufikia tarehe 2/4/2017 jumla ya hati 9 zilikuwa zimesajiliwa na kuletwa Mkoani na wananchi wenye hati hizo walijulishwa kwenda kuchukua hati zao.
**Hoja:** Ni lini wananchi watapewa hati miliki za maeneo wanayoishi?

**Ufafanuzi:** Hati miliki zinatolewa na kamishina kwenye maeneo yaliyopimwa, kwa upande wa vijiji zinatolewa hati miliki za kimila.

**Hoja**: Wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2017 waripoti shuleni na kupata mrejesho kabla ya tarehe 13/02/2017
**Utekelezaji**: Taarifa ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2017ni kama ifuatavyo:-

i) Waliochaguliwa ni 3316
ii) Walioripoti ni 2529 (76.27%)
iii) Waliohama ni 317 (9.56%)
iv) Walioenda shule binafsi ni 346 (10.43%)
v) Wasioripoti shuleni ni 124 (3.74%)

Taarifa kwa kina imeambatanishwa (kiambatanisho A)

**Hoja**: Kaya zote ambazo hazina vyoo bora ziwe na vyoo kufikia tarehe 30 Juni, 2017
**Utekelezaji**: Agizo limezingatiwa unaandaliwa utaratibu wa kuhakikisha kila kaya kuwa na choo bora kufikia tarehe 30 Juni, 2017
**HOJA**: Maafisa watendaji wa kata watembelee kaya kwa kaya na kuhimiza kutunza chakula kwa matumizi ya baadae.
**UTEKELEZAJI**: Iliandikwa barua yenye Kumb Na. BA.349/23/13/6 ya tarehe 08/02/2017 ikiwaagiza watendaji wa kata kwa kushirikiana na maafisa kilimo, watendaji wa vijiji na wenyeviti wa vitongoji kutembelea kaya kwa kaya kuhimiza kutunza chakula kinachovunwa kwa matumizi ya baadae.
Malengo ya Mavuno ya zao la mahindi kwa msimu wa vuli mwaka 2016/2017 yalikuwa tani 105,600. Kiasi cha mahindi yaliyovunwa ni takribani tani 66,318**,** mahitaji ya chakula kwa kaya zote 53,504 za wilaya ya Kyerwa ni tani 30,180 kwa kipindi cha miezi 6. Mahindi yaliyosafirishwa kwenda kuuzwa nje ya Wilaya yakiwa ni chakula cha ziada tangu Januari hadi mwezi Machi mwaka 2017 jumla ya magunia 18,363 sawa na tani 1742**.** Kiasi cha tani 34,396 zinakadiriwa kuwa bado zipo.
Baada ya majadiliano taarifa ilipokelewa.

**KUMB NA 31/2016/2017 KUPOKEA TAARIFA YA UTENDAJI WA UWAJIBIKAJI WA HALMASHAURI KUTOKA KWA WENYEVITI WA KAMATI ZA KUDUMU KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU 2016/2017**

Taarifa za kamati za kudumu ziliwasilshwa kama ifuatavyo:-

**i. Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango**

Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji ni kwa nini malando yasipelekwe kwenye kata zote? Ilijibiwa kuwa malando yalitolewa kwenye kata zilizoathirika zaidi na kwa kuwa mvua zinaendelea kunyesha wasambaze mbegu kwa wengine ili zipatikane za kutosha.

Baada ya majadiliano taarifa ilipokelewa.

ii. Kamati ya Elimu, Afya na Maji. Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa
iii. Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira .Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.

iv. Kamati ya kudhibiti UKIMWI. Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.

**KUMB NA 32/2016/2017 TAARIFA ZA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA**

1. **Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2016/2017**

Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kama ifuatavyo:-

**Hoja**: Kuna mkakati gani wa kumaliza tatizo la kuweka fedha akaunti tofauti za vijiji?

**Ufafanuzi**: Fedha ya utekelezaji wa miradi katika vijiji inapowekwa benki haina makato yoyote, pia kuweka akaunti tofauti ni kwamba akaunti zote zinaletwa kutoka vijijini, hivyo wanapaswa kuwa makini wakati wa kuwasilisha akaunti za vijiji. Ilisisitizwa kuwa watendaji wa kata wahakikishe fedha inapotolewa inatumika kwa wakati.

**Hoja**: Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji itasaidiaje kwenye udharula wa choo ya taasisi kutitia kabla ya kibali cha kuruhusu kuchangisha kutolewa.

**Ufafanuzi:** Choo ikianza kujaa viongozi wajipange na kufanya vikao kwa ajili kuweka choo mbadala kabla ya choo kutitia. Ulitolewa ushauri wa kujenga choo nje ya shimo ili kuzuia kutitia kwa vyoo.

Baada ya taarifa kuwasilishwa ilipokelewa.

2. **Taarifa ya ukaguzi wa ndani kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa kwa robo ya tatu Januari hadi Machi, 2017.**

Kwa robo ya tatu Januari hadi Machi, 2017 jumla ya hoja 9 za ukaguzi zilijitokeza. Kati ya hoja hizo 9, hoja 1 imepatiwa majibu na kufungwa baada ya utekelezaji kufanyika. Hoja 8 zilizobaki zinasubiri utekelezaji. Aidha kitengo cha ukaguzi wa ndani kilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji kwa hoja za robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2016 ambapo hoja sita zilizobaki zilifungwa baada ya utekelezaji.

Taarifa ilipokelewa.

3. **Taarifa ya manunuzi na bodi ya zabuni kwa robo ya tatu kuanzia Januari hadi Machi, 2017**

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ya Wilaya imekisia kununua vifaa, kazi za kihandisi na huduma mbalimbali zenye thamani ya Tshs. 7,547,351,843 kwa mwaka. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017 Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa imefanya manunuzi yenye thamani ya Tshs.1,573,912,283 ikiwa ni asilimia 20.85 ya manunuzi yote yanayotarajiwa kufanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa kipindi cha robo ya tatu pekee Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa imefanya manunuzi yenye thamani ya Tshs. 299,529,230 yenye mchanganuo ufuatao:-

Vifaa na huduma Tshs 20,042,521, mafuta dieseli Tshs.20,596,100, madawa na vifaa tiba Tshs. 152,665,990, kazi za kihandisi Tshs. 92,648,119 na ununuzi wa matairi Tshs. 13,576,500.

4. **Taarifa ya kitengo cha sheria Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa kwa robo ya tatu 2016/2017 na mabaraza ya kata.**

Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kama ifuatavyo:-

Lilitolewa ombi la kupatiwa miongozo ya baraza la kata. Ilielezwa kuwa miongozo ilishatolewa kwenye kata.

**Hoja**: Ni lini Mabaraza ya kata watapewa semina.

**Ufafanuzi**: Semina zimetolewa kwa kata 12 na miongozo kuhusu kata ambazo hazijawasilisha majina yakiwasilishwa semina zitatolewa.

**KUMB NA 33/2016/2017 TAARIFA ZINGINEZO MUHIMU**

a. **Taarifa ya hali ya usalama**

Taarifa iliwasilishwa kama ifuatavyo:-

**Hali ya uhalifu**.

Kwa mwaka 2016 zilitokea kesi za ubakaji 3, wizi wa mifugo, makosa ya mauaji, dawa za kulevya na makosa ya magendo.

- Makosa ya barabarani kwa mwezi Februari yalikuwa makosa 39
- Unyang'anyi wa silaha walikamatwa watu 5 na uchunguzi unaendelea
- Tukio la kuzama kwenye maji miili ya watu wawili (2) katika mto Kagera miili hiyo ilipatikana.

Changamoto.

- Ukosefu wa makazi ya polisi
- Idadi ya watumishi iliyopo haikidhi mahitaji
- Kukosa kituo cha Polisi chenye hadhi

**Hoja**: Mwaka 2007 ilitolewa ardhi kujenga kituo cha polisi eneo la Nkwenda je, ufuatiliaji umefikia wapi wa kujenga kituo hicho?

**Ufafanuzi**: Wananchi wanapaswa kuchangia ili kuanzisha ujenzi na mawasiliano yalishafanyika ni kusubiri kuanza. Ulitolewa ushauri kwa Mheshimiwa Diwani wa Nkwenda kufuatilia kwa ukaribu ili eneo liweze kujengwa.

Ilielezwa kuwa matukio katika kata ya Nyarozumbura ni mengi kama vile kuvamia, kunyang'anya na kuvunja maduka ambapo maduka 6 yalivunjwa na watu wasiojulikana.

Lilitolewa ombi la kupata kituo cha polisi kwenye migodi wa Sindiketi- Kyerwa. Ilijibiwa kuwa ombi lilishatolewa kwa wahusika ili kuruhusu kupewa kituo cha polisi katika eneo la mgodi. Pia doria zinafanyika katika maeneo hayo ili kuweka usalama zaidi askari polisi kutoka kituo cha polisi Kagenyi.

Baada ya majadiliano taarifa ilipokelewa.

ii. **Idara ya uhamiaji**

Afisa uhamiaji alieleza tafsiri halisi ya maana uhamiaji haramu. Aidha alitoa aina 4 za uraia ambazo ni uraia wa kuzaliwa, uraia wa kurithi, uraia wa kuandikishwa na uraia wa ulaifa.

Raia akizaliwa Tanzania na akafikisha miaka 18 anapaswa kupata uraia wake wa kuwa raia Tanzania.

Ilielezwa kuwa watu wasiyo raia wa Tanzania wanaendelea kubainiwa kwa kuhakikisha kila raia wa Tanzania ana:

- Cheti cha kuzaliwa kinachobainisha uraia wake. Pia huduma za NIDA zoezi linaendelea vizuri.

**Hoja:** Kama mtoto amepata cheti cha chuo kinaandikwa mtanzania na wazazi siyo raia itakuwaje?

**Ufafanuzi:** Watoto waliozaliwa kabla ya kupata uraia, mtoto anaomba uraia baada ya kufikisha miaka 18. Kama ameishapata mtoto anakuwa raia au kuishi kwa mkataba.

Watakaoingia ndani ya kata ambao siyo raia wa Tanzania wabainishwe na kurudishwa kwao, endapo ni raia wa Tanzania anahamia sehemu nyingine anapaswa kufuata taratibu zote zinazotakiwa za kumtambulisha kutoka kwa viongozi wa eneo husika.

**KUMB NA 34/2016/2017 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe walivyojadili agenda zilizowasilishwa na kusisitiza kutekeleza yote yaliyoazimiwa. Baada ya kusema hayo alifunga kikao mnamo saa 11:20 jioni.

Saini.......................... Saini..........................

Jina SHADRACK M. MBAGAMA Jina KASHUNGU S.R

Katibu Mwenyekiti

Tarehe 22.08.2017